# SAUTI YA TSC

TOLEO NA.13 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) MACHI 2022

## WAZIRI BASHUNGWA AWATAKA WAKUU WA SHULE KUSIMAMIA MIRADI KWA UFASAHA




*WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa akizungumza wakati wa hafla ya Utoaji wa Tuzo za Ubora wa Taaluma kwa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa Mwaka 2021 iliyofanyika Februari 11, 2022 jijini Dodoma.*

**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
**Simu:** +255 (26) 2322402-4 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz **Tovuti:** www.tsc.go.tz

# RAIS AMETUJENGEA MADARASA, SASA TUIHIMIZE JAMII KUPELEKA WATOTO SHULE KWA WAKATI

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wetu mpendwa, Mhe. Samia Suluhu Hassan imefanya jitihada kubwa za kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu nchini ikiwa ni moja ya mikakati yake ya kuifanya sekta ya elimu kupiga hatua zaidi na kulifanya Taifa letu kufikia malengo yake katika maendeleo.

**“Ujenzi wa miundo mbinu hiyo umesaidia kutatua changamoto iliyokuwepo kwa muda mrefu ya upungufu wa vyumba vya madarasa uliokuwa unasababisha wanafunzi kwenye baadhi ya shule kurundikana kwenye darasa moja...”**

Hivi karibuni tumeshuhudia fedha nyingi zikitumika katika kuimarisha miundombinu mbalimbali ya shule ikiwemo ujenzi wa vyumba vya madarasa kote nchini ili kuweka mazingira mazuri ya utoaji elimu.

Ujenzi wa miundo mbinu hiyo umesaidia kutatua changamoto iliyokuwepo kwa muda mrefu ya upungufu wa vyumba vya madarasa uliokuwa unasababisha wanafunzi kwenye baadhi ya shule kurundikana kwenye darasa moja wakati wa masomo na hata wengine kusomea chini ya miti kitu ambacho kilikuwa kinarudisha nyuma maendeleo ya elimu.

Baada ya kazi nzuri ya ujenzi wa miundombinu kufanyika wadau wa elimu tuna kila sababu ya kuhamasisha wazazi, walezi na jamii kwa ujumla ili kila mtoto anayestahili kwenda shule apate haki hiyo kikamilifu.

Kwa upande wa walimu, miundombinu hiyo pia inapaswa kutupa ari na hamasa ya kufanya kazi kwa bidii, weledi na uzalendo zaidi katika kutoa huduma bora kwa wanafunzi ili tuendelee kujenga Taifa bora.


## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina Nkwama

**Wajumbe**
Moses Chitama
Christina Hape
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya

**Mhariri Mkuu**
Gerard Chami

**Mhariri**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon


## KATUNI




**Wasiliana nasi kwa Simu:** +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***

# WAZIRI BASHUNGWA AWATAKA WAKUU WA SHULE KUSIMAMIA MIRADI KWA UFASAHA



*WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa akizungumza wakati wa hafla ya Utoaji wa Tuzo za Ubora wa Taaluma kwa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa Mwaka 2021 iliyofanyika Februari 11, 2022 jijini Dodoma.*

**Na. Mwandishi Wetu - Dodoma**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mita (TAMISEMI), Innocent Bashungwa amewataka wakuu wa shule nchini kusimamia miradi ya shule kwa ufasaha ili iendane na thamani ya fedha zilizotolewa na Serikali.

Waziri Bashungwa ameyasema hayo hivi karibuni jijini Dodoma kwenye hafla ya utoaji wa Tuzo za Ubora wa Taaluma kwa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa Mwaka 2021 kwa mikoa 26 ya Tanzania bara.

Alisema ili kufikia malengo ya serikali ni lazima kusimamia miradi yote kwa ufasaha na kuhakikisha inaendana na thamani ya fedha,



*Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, David Silinde akizungumza wakati wa hafla ya Utoaji wa Tuzo za Ubora wa Taaluma kwa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa Mwaka 2021 iliyofanyika Februari 11,2022 jijini Dodoma.*

na mali za shule zitunzwe vizuri ili ziweze kudumu kwa muda mrefu.

"Natoa maagizo kwa Wakuu wote wa Shule nchini kuhakikisha kwamba wanasimamia sheria, miongozo na taratibu katika sekta ya elimu, kusimamia miradi yote inayotekelezwa katika maeneo yao, pamoja na kutunza majengo ili yatumike hata katika vizazi vijavyo," alisema Bashungwa.

"Wapo baadhi yenu ambao hamna uhusiano mzuri na jamii hivyo hukwamisha utekeleaji wa shughuli za serikali hasa miradi, mnapokuwa na uhusiano mzuri na viongozi katika jamii inarahisisha katika utekelezaji na hata utunzaji wa majengo ya serikali," alisema Bashungwa.

Kwa upande wake Kaimu Rais wa Chama Cha Walimu Tanzania (CWT) Mwalimu, Dina Mathamani amesema wao kama walimu wameona umuhimu wa kutoa tuzo na pongezi kwa walimu waliofanya vizuri na kuwafanikisha wanafunzi kufaulu vizuri.

"Ufaulu unaendelea kupanda siku hadi siku taaluma zinapanda na mazingira ya walimu yataendelea kuboreshwa na niahidi kwa niaba ya Chama cha Walimu kuwa tutafanya kazi kwa weledi na kuhakikisha ufaulu unaongezeka ili tupate wataalamu katika sekta mbalimbali" alisema Mwl. Mathamani.

Awali Katibu Mkuu wa Chama Cha Walimu Tanzanaia (CWT), Mwalimu Deus Seif alisema Chama hicho kinatambua jitihada kubwa zinazofanywa na serikali

# WAZIRI BASHUNGWA AWATAKA WAKUU WA SHULE KUSIMAMIA MIRADI KWA UFASAHA



*MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka akitoa salamu za Mkoa wakati wa hafla ya Utoaji wa Tuzo za Ubora wa Taaluma kwa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa Mwaka 2021 iliyofanyika Februari 11, 2022 jijini Dodoma.*



*Kaimu Rais wa Chama Cha Walimu Tanzania (CWT), Mwl. Dina Mathamani akizungumza wakati wa hafla ya utoaji wa Tuzo za Ubora wa Taaluma kwa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa Mwaka 2021 iliyofanyika Februari 11, 2022 jijini Dodoma.*





*Sehemu ya walimu pamoja na wanafunzi wakifatilia hotuba mbalimbali wakati wa hafla ya Utoaji wa Tuzo za Ubora wa Taaluma kwa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa Mwaka 2021 iliyofanyika Februari 11, 2022 jijini Dodoma.*

katika kuboresha maisha ya watanzania wakiwemo walimu.

Aidha, Mwl. Seif ameiomba serikali kulipa madai ya walimu wanayodai kupitia Halmashauri mbalimbali ili kuongeza ari ya kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi zaidi.

"Pia kuna madai mbalimbali ya walimu bado yapo katika Halmashauri zetu na hata wizarani, likizo, matibabu, uhamisho, malimbikizo ya mishahara na madaraja. Tunaomba uhakiki wa mara kwa mara ufanyike na walimu walipwe ili kuongeza ari ya kufanya kazi," amesema

# WAZIRI BASHUNGWA AWATAKA WAKUU WA SHULE KUSIMAMIA MIRADI KWA UFASAHA

Pamoja na hayo, Kiongozi huyo aliiomba Serikali kuendelea kujenga nyumba za walimu hasa wa maeneo ya pembezoni ambapo kuna shida zaidi ya nyumba ili kuwaondoa walimu katika adha ya kutembea umbali mrefu kufika shuleni.

Hafla hivyo ya utoaji wa Tuzo hizo za Ubora wa Taaluma kwa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa Mwaka 2021 ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwemo Katibu wa Tume ya utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, akikabidhi tuzo kwa mmoja wa walimu wakati wa hafla ya utoaji wa Tuzo za Ubora wa Taaluma kwa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa Mwaka 2021 iliyofanyika Februari 11, 2022 jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, akikabidhi medali kwa mmoja wa wanafunzi wakati wa hafla ya utoaji wa Tuzo za Ubora wa Taaluma kwa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa Mwaka 2021 iliyofanyika Februari 11, 2022 jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, akikabidhi medali kwa mmoja wa wanafunzi wakati wa hafla ya utoaji wa Tuzo za Ubora wa Taaluma kwa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa Mwaka 2021 iliyofanyika Februari 11, 2022 jijini Dodoma.*

# KATIBU MKUU WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI ZANZIBAR AIPONGEZA TSC KWA KUSIMAMIA NIDHAMU YA WALIMU

**Na. Mwandishi Wetu - Zanzibar**

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis ameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kuendelea kusimamia nidhamu na maadili ya walimu kwa ufanisi kitu ambacho kimesaidia kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu wa wanafunzi nchini.



*Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis akiongea na viongozi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (kushoto) na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (kulia). Mazungumzo hayo yalifanyika ofisini kwa Katibu Mkuu huyo mjini Unguja hivi karibuni.*

Kiongozi huyo aliipongeza TSC kwa nyakati tofauti, wakati viongozi wa TSC wakiongozwa na Mwenyekiti na Katibu wa tume hiyo walipomtembelea ofisini kwake na Katibu Mkuu huyo alipotembelea Mkutano wa Tume uliokuwa unafanyika katika ukumbi wa jengo la Mamlaka ya Udhibiti Huduma za Maji na Nishati (ZURA) visiwani Zanzibar hivi karibuni.

Bw. Khamis alisema TSC imekuwa kielelezo bora kutokana na utendaji wake wa kazi wa kusimamia maadili na nidhamu ya walimu na hivyo kusaidia wanafunzi kupata haki yao ya msingi ya kufundishwa kikamilifu na kuifanya sekta ya elimu kuendelea kuwa na maendeleo mazuri.

"Maendeleo mazuri ya taaluma ya mwanafunzi yanasababishwa na walimu wanaowajibika, walimu wasipokuwa na nidhamu na maadili katika utendaji wao wa kazi ni wazi kuwa viwango vya taaluma kwa wanafunzi vitaporomoka. Usimamizi wa walimu mnaoufanya kwa kiasi kikubwa unasaidia wanafunzi kupatiwa haki yao ya kufundishwa," alisema kiongozi



*Makamisha pamoja na Wakurugenzi wa TSC wakiendelea kufuatilia mazungumzo kati ya Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba pamoja na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama. Mazungumzo hayo yalifanyika ofisini kwa Katibu Mkuu huyo mjini Unguja hivi karibuni.*

# KATIBU MKUU WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI ZANZIBAR AIPONGEZA TSC KWA KUSIMAMIA NIDHAMU YA WALIMU



*Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba akiteta jambo na Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis nje ya jengo la Wizara hiyo visiwani Zanzibar.*



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama akiteta jambo na Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis nje ya jengo la Wizara hiyo visiwani Zanzibar.*



*Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis akiongea na Makamishna pamoja na Sekretarieti ya TSC (hawapo pichani) wakati alipotembelea mkutano wa tume hiyo uliokuwa ukifanyika katika ukumbi wa jengo la Mamlaka ya Udhibiti Huduma za Maji na Nishati (ZURA) visiwani Zanzibar hivi karibuni. Wengine ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (katikati) na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (kushoto).*

huyo.

Akizungumzia usimamizi wa maadili na nidhamu ya walimu visiwani hapo, Katibu Mkuu huyo alisema Zanzibar bado haijawa na chombo mahsusi kama ilivyo TSC, badala yake Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ndiyo inayosimamia masuala yote ya elimu na walimu huku akieleza kuwa ipo haja ya wao kuanzisha chombo hicho ili kuongeza ufanisi wa usimamizi wa masuala ya walimu.

Aliongeza kuwa pamoja na kwamba taaluma kwa wanafunzi visiwani hapo ni nzuri bado kuna umuhimu wa kuwa na chombo cha kusimamia maadili ya walimu kuanzia ngazi za chini ili iwe rasihi kumrekebisha mwalimu mapema pale anapokwenda kinyume na maadili ya kazi yake.

"Nilijaribu kufuatilia kwenye shule za wilaya mbalimbali kujua sababu zinazofanya wanafunzi

# KATIBU MKUU WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI ZANZIBAR AIPONGEZA TSC KWA KUSIMAMIA NIDHAMU YA WALIMU



*Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis akiongea na Makamishna pamoja na Sekretarieti ya TSC wakati alipotembelea mkutano wa tume hiyo uliokuwa ukifanyika katika ukumbi wa jengo la Mamlaka ya Udhibiti Huduma za Maji na Nishati (ZURA) visiwani Zanzibar hivi karibuni.*

wasifanye vizuri katika mitihani yao. Mwanzoni tulifikiri sababu kubwa ni upungufu wa walimu na mlundikano wa wanafunzi darasani. Tulipoangalia wilaya moja moja tuligundua kuwa zile zinazoonekana zina wanafunzi wengi bado wamefanya vizuri kuliko maeneo yenye wanafaunzi wachache darasani na zile shule zenye walimu wengi tuliona bado hawakufanya vizuri sana. Mwisho tukagundua kwamba tatizo kubwa lipo kwenye nidhamu na uwajibikaji wa walimu wetu. Hivyo, tunaendelea kuangalia namna nzuri zaidi itakayosaidia kusimamia maadili ya walimu kwa karibu" alisema.

Viongozi hao wa TSC walipata fursa ya kumwelezea Katibu Mkuu huyo namna TSC inavyofanya kazi kuanzia ngazi ya shule hadi ngazi ya Makao Makuu na namna mamlaka hiyo inavyoendesha mashauri ya nidhamu pamoja na rufaa zinazowahusu walimu.




*Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis (wa tatu kutoka kulia mstari wa mbele) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kulia mstari wa mbele, mwenye tai nyeupe), Katibu wa TSC Paulina Nkwama (wanne kutoka kushoto). Wengine ni Makamishana pamoja na Wakurugenzi wa TSC.*

# KATIBU MKUU WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI ZANZIBAR AIPONGEZA TSC KWA KUSIMAMIA NIDHAMU YA WALIMU



*Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis (wa pili kutoka kulia kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa tatu kutoka kulia kwa waliokaa), Katibu wa TSC Paulina Nkwama (wanne kutoka kulia kwa waliokaa), Mwenyekiti Msaidizi wa TSC, Bahati Mgongolwa (wa kwanza kulia kwa waliokaa) na Mkurugenzi wa Elimu Sekondari wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Asya Iddi Issa (wa kwanza kushoto kwa waliokaa). Wengine ni Makamishana wa TSC pamoja na Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa TSC, Moses Chitama (wa kwanza upande wa kushoto kwa waliosimama).*



*Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis (wa pili kutoka kulia kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa tatu kutoka kulia kwa waliokaa), Katibu wa TSC Paulina Nkwama (wanne kutoka kulia kwa waliokaa), Mwenyekiti Msaidizi wa TSC, Bahati Mgongolwa (wa kwanza kulia kwa waliokaa) na Mkurugenzi wa Elimu Sekondari wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Asya Iddi Issa (wa kwanza kushoto kwa waliokaa). Wengine ni Makamishna na Sekretarieti ya TSC.*

# KUTOSHIRIKISHWA MAANDALIZI YA MIPANGO YA MAFUNZO KWA WALIMU, KIKWAZO KATIKA UTEKELEZAJI WA JUKUMU LA KISHERIA LA AJIRA NA MAENDELEO YA WALIMU – TSC MASASI




*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami akiongea na Watumishi wa TSC Wilaya ya Masasi wakati wa ziara yake wilayani hapo iliyofanyika hivi karibuni kwa lengo la kufahamu maendeleo ya ofisi hiyo katika kutoa huduma kwa walimu.*

**Na. Mwandishi Wetu – Masasi**

Hali ya kutoshirikishwa katika maandalizi ya mipango kazi ya mafunzo kwa walimu inayoendana na bajeti na ikama kumebainika kuwa sehemu ya kikwazo katika utekelezaji kwa ufasaha wa jukumu la kisheria la Ajira na Maendeleo ya Walimu katika Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilayani Masasi, Mkoani Mtwara inayohudumia Halmashauri mbili; Masasi Wilaya na Masasi Mji.

Akizungumza na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali Tume Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, hivi karibuni akiwa ziarani katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, na Morogoro, kwa niaba ya Kaimu Katibu Msaidizi (KKM) wa TSC Masasi, Mwl. Chama Hokororo; Mwl. Delaide Mrope, alisema; Mipango ya mafunzo huandaliwa na Halmashauri husika ambayo hutambulika kama mwajiri huku jukumu la maendeleo ya walimu hao na msawazo baada ya ajira zao likiwa chini ya TSC ambao wanapaswa kushirikishwa na kushauri katika mipango hiyo ya mafunzo kila mwaka kusaidia kutoathiri maendeleo hayo ya walimu na utoaji elimu kwa ujumla vituoni.

"Pamoja na kukumbushana mara kwa mara na wenzetu wa Halmashauri juu ya jukumu letu la kisheria kwenye ajira na maendeleo ya walimu baada ya ajira zao lakini bado tumekua tukikabiliwa na changamoto kubwa sana ya kutoshirikishwa katika maandalizi ya mipango ya mafunzo na bajeti zinazowahusu walimu tunaowahudumia. Ni




*Afisa Ajira na Maendeleo ya Walimu wa TSC Wilaya ya Masasi, Delaide Mrope akielezea hatua iliyofikiwa na ofisi hiyo katika kutoa huduma kwa walimu wakati wa kikao cha watumishi wa TSC wilayani hapo na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu kilichofanyika hivi karibuni. Kushoto ni Afisa wa TSC Wilaya ya Masasi, Muksin Mussa na upande wa kulia ni Katibu Muhtasi wa TSC Wilaya ya Masasi, Ziada Milanzi.*

# KUTOSHIRIKISHWA MAANDALIZI YA MIPANGO YA MAFUNZO KWA WALIMU, KIKWAZO KATIKA UTEKELEZAJI WA JUKUMU LA KISHERIA LA AJIRA NA MAENDELEO YA WALIMU – TSC MASASI



*Watumishi wa TSC Wilaya ya Masasi Delaide Mrope (katikati), Muksin Mussa (kushoto) na Ziada Milanzi (kulia) wakimsikiliza Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani) wakati wa kikao cha watumishi hao na kiongozi huyo kilichofanyika hivi karibuni Wilayani Masasi.*

wito wetu kwao tunaendelea kuwakumbusha kuishirikisha Ofisi ya TSC Wilaya katika maandalizi ya mipango hii ili kushauriana na kutoka na mipango iliyo bora kwetu sote na inayotekelezeka bila changamoto kwani tunapaswa kuzungumza lugha moja na kutembea pamoja kulisukuma gurudumu hili la Elimu nchini." Alisema Mwl. Mrope

Kwa niaba ya KKM Hokororo, Mwl. Mrope alisema wanajivunia kwa kiwango kikubwa Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu kuendelea kufuatilia kwa karibu, kusimamia na kuwezesha maendeleo ya watumishi vituoni mwao kwa yale yaliyo chini ya mamlaka zao kisheria kwani yanapunguza malalamiko na kuongeza tija ya uwajibikaji kwa walimu.

Aidha, Mwl. Mrope alisema Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi umekua na ushirikiano mkubwa na Ofisi ya TSC Wilaya ya Masasi katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali yanayoihusu sekta ya Elimu wakiwamo walimu ikiwamo kushirikishwa katika vikao mbalimbali muhimu vya maamuzi na mashauriano pamoja na kuipatia Tume ofisi kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu na kuonana na wateja na wadau wa Tume tofauti na Halmashauri ya Mji Masasi ambao wamekua wazito sana katika kutoa ushirikiano na hivyo kuleta ugumu mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Tume wilayani katika eneo hilo la mji.

Kwa niaba ya KKM Hokororo, Mwl. Mrope alitoa rai kwa Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na Halmashauri ya Mji Masasi kuwakabidhi walimu barua na mikataba ya ajira kwa wakati kwani sehemu kubwa ya wateja wao wanaowahudumia mpaka sasa wamepokea barua za ajira wakisubiri kwa kipindi kirefu mikataba ya ajira na hivyo kushusha ari ya uwajibikaji wa walimu kutokana na kutokua na mikataba hiyo.

Ofisi ya TSC Wilayani Masasi, Mkoani Mtwara inahudumia Halmashauri mbili ya Masasi Wilaya na Masasi Mji zikiwa na jumla ya shule 205 ambazo kati yake Shule za Msingi ni 168, Sekondari 37, na Shikizi sita (Liurungu, Pachani, Namatutwe, Namaunya, Mkajamila, na Nangose Juu), zikihudumiwa na jumla ya Walimu 1,826 (Wanaume 1,049 na Wanawake 777) ambao kati yao; Walimu 1,300 (Wanaume 691 na Wanawake 609) wanafundisha Shule za Msingi huku Walimu 526 (Wanaume 359 na Wanawake 167) wakiwa wanafundisha Shule za Sekondari.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali na Habari kutoka Ofisi ya Rais – Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami yupo katika mwendelezo wa ziara za Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali na Habari za kila mwezi kutembelea Ofisi za TSC Wilaya zilizopo katika wilaya 139 hapa nchini ili kujionea uwajibikaji na kupata taarifa za utekelezaji wa majukumu ya TSC Wilaya pamoja na kutoa elimu zaidi ya uelewa wa majukumu ya TSC kwa wadau mbalimbali wa Tume.

# TUZO ZA UBORA WA TAALUMA KWA MATOKEO YA MITIHANI YA ELIMU YA MSINGI NA SEKONDARI ZAFIKISHWA ZANZIBAR

**Na Mwandishi Wetu - Zanzibar**

Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Awali na Msingi kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambaye pia ni Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Suzana Nussu amekabidhi Tuzo za Ubora wa Taaluma kwa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa Mwaka 2021 kwa upande wa Zanzibar.

Kiongozi huyo alikabidhi tuzo hizo hivi karibuni visiwani Zanziabar huku akieleza kuwa zoezi la kukabidhi tuzo hizo kitaifa ilifanya na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Innocent Bashungwa Februari 11, 2022 huku akieleza kuwa kwa upande



*Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia Elimu ya Awali na Msingi kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Suzana Nussu akiwa ameshikilia moja ya Tuzo za Ubora wa Taaluma kwa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa Mwaka 2021 tayari kwa kuikabidhi kwa Mkurugenzi wa Elimu Sekondari kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Asya Iddi Issa (hayupo pichani) hivi karibuni mjini Zanzibar.*



*Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia Elimu ya Awali na Msingi kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Suzana Nussu akikabidhi moja ya vyeti vya ubora wa taaluma kwa Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Asya Iddi Issa.*

# TUZO ZA UBORA WA TAALUMA KWA MATOKEO YA MITIHANI YA ELIMU YA MSINGI NA SEKONDARI ZAFIKISHWA ZANZIBAR



*Mkurugenzi wa Elimu ya Sekondari kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Awali Zanzibar, Asya Iddi Issa akitoa neno la Shukrani mara baada ya kupokea tuzo za ubora kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi wa Elimumu ya Awali na Msgingi, Suzana Nussu (hayupo pichani) kutoka TAMISEMI. Pembeni ya Mkurugenzi huyo ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba.*

wa Zanzibar hapakuwa na mwakilishi.

Akipokea tuzo hizo kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Mkurugenzi wa Elimu Sekondari wa Wizara hiyo, Bi. Asya Iddi Issa alisema kuwa kutambua walimu hasa pale wanapofanya vizuri katika kazi zao ni jambo jema ambalo linawatia moyo kuendelea kujituma na hivyo kuendelea kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi.

"Kwa kweli mmebuni kitu kizuri, kutambua juhudi ya mtu hasa pale anapofanya vizuri inampa hamasa ya kuendelea kufanya kazi kwa weledi na ufanisi zaidi. Hivyo, ninawashukuru kwa medali na vyeti hivi ambavyo mmevitoa kwa walimu wetu waliofanya vizuri katika majukumu yao. Ninaahidi kuwa medali na vyeti hivi vitaendelea kuwa chachu zaidi katika kutoa elimu kwa wanafunzi," alisema Mkurugenzi huyo.

# TSC KIBITI YAJIVUNIA JUHUDI YA UTOAJI ELIMU KWA WALIMU NA WANAFUNZI ILIYOPUNGUZA MASHAURI YA WALIMU WILAYANI HUMO

**Na. Mwandishi Wetu – Kibiti**

Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilayani Kibiti, Mkoani Pwani inayohudumia Halmashauri moja ya Wilaya ya Kibiti; inajivunia kutoa elimu kwa sehemu kubwa ya walimu katika halmashauri hiyo kuhusiana na masuala ya Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo, Nguzo za Kazi ya Ualimu, na utekelezaji wa zoezi la tathmini ya utendaji kazi na utekelezaji wa majukumu yaani OPRAS.

Hilo lilibainika hivi karibuni wakati wa mazungumzo ya Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami na Kaimu Katibu Msaidizi (KKM) wa TSC - Kibiti, Ndg. Masoud Habib, wakati wa ziara za kila mwezi za Mkuu huyo wa Mawasiliano na Habari kutembelea Ofisi za TSC Wilaya ikiwa ni sehemu ya mwendelezo wa ziara hizo 139 hapa nchini ili kupata taarifa za utekelezaji wa majukumu ya TSC Wilaya pamoja na kutoa elimu zaidi ya uelewa wa majukumu ya TSC.

"Tumefanikiwa na tunaendelea kutoa elimu kwa walimu wote tunaowahudumia katika halmashauri yetu kuhusiana na masuala ya Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo, Nguzo za Kazi ya Ualimu, utekelezaji wa zoezi la tathmini ya utendaji kazi na utekelezaji wa majukumu yaani OPRAS lakini pia tunatoa elimu mtambuka kwa walimu wetu kuhusiana na mapambano dhidi ya rushwa, UVIKO-19, VVU na UKIMWI, athari za madawa ya kulevya na mimba za utotoni kwa wanafunzi pamoja na kushinikizana kushiriki kwa uzalendo mkubwa katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi." Alisema Ndg. Habib

KKM Habib alisema pamoja na elimu hiyo ofisi yao imefanikiwa kuwafikia walimu katika maeneo wanayofanyia kazi licha ya uwepo wa changamoto za miundombinu mibovu na jografia ya wilaya isiyo rafiki kuweza kufika katika baadhi ya vituo na kutatua baadhi ya changamoto zinazowakabili walimu katika utendaji wao wa kazi ndani ya wilaya na hivyo kupunguza sehemu kubwa madhara yanayoweza kuwapata katika utumishi wao kutokana na utoro, matumizi ya vileo, mahusiano ya mapenzi kazini, na nyinginezo.

Alizitaja sehemu ya changamoto zinazowakabili



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kibiti, Ali Masoud (kushoto) akitoa ufafanuzi wa taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya TSC katika Wilaya hiyo kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami kutoka TSC Makao Makuu.*



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kibiti, Ali Masoud (kushoto) na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami kutoka TSC Makao Makuu wakipitia baadhi ya nyaraka za utekelezaji wa majuku ya TSC Wilaya ya Kibiti hivi karibuni.*

# TSC KIBITI YAJIVUNIA JUHUDI YA UTOAJI ELIMU KWA WALIMU NA WANAFUNZI ILIYOPUNGUZA MASHAURI YA WALIMU WILAYANI HUMO



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami kutoka TSC Makao Makuu (kulia) akizungumza na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Kibiti, Ali Masoud wakati mkuu huyo wa kitengo alipofanya ziara katika ofisi ya TSC Wilaya ya Kibiti hivi karibuni.*



*Afisa Nidhamu na Maadili wa TSC Wilaya ya Kibiti, Mwashamba Mbuyita akiwa ofisni kwake.*

walimu kuwa ni pamoja na; uwepo wa tuhuma zinazowakabili walimu wa shule za sekondari kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi wa kike, walimu kufanya kazi katika kituo kimoja kwa muda mrefu wengine kufikisha miaka 21 katika kituo kimoja, uchelewaji wa malipo ya fedha za likizo hasa elimu sekondari, na uchelewaji wa malipo ya fedha za kufungasha mizigo kwa wastaafu.

Aidha, KKM Habib alisema pamoja na hali ya nidhamu kuendelea kuimarika kutokana na juhudi za TSC katika utoaji elimu kuendelea wilayani humo kwa kushirikiana na Idara ya Udhibiti Ubora na wadau wengine muhimu, jumla ya mashauri matatu yameshapokelewa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2021/ 22 ambayo yote yanahusiana na udanganyifu katika mitihani iliyopita ya darasa la saba na yote yameshahitimishwa kwa mmoja kushushwa cheo, mmoja kupunguziwa mshahara na mmoja kubainika hana hatia.

Pia alisema mwenendo wa mashauri umeendelea kushuka mwaka hadi mwaka kutokana na juhudi hizo za pamoja na uelimishaji na ufuatiliaji wa walimu vituoni kwani katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/ 18 jumla ya mashauri sita (6) yalipokelewa, kushughulikiwa na kuhitimishwa huku mwaka 2018/ 19 yakipokelewa na kuhitimishwa mashauri sita (6), mwaka 2019/ 20 mashauri matatu (3), na mwaka 2020/ 21 shauri moja (1).

Vilevile KKM huyo wa TSC - Kibiti alisema katika halmashauri wanayoihudumia walimu wote 399 sawa na asilimia 100 waliokuwa na sifa za kupanda cheo ndani ya ikama ya jumla ya 1446 walipandishwa cheo na kuanza kupokea mishahara mipya baada ya kuingizwa kwenye mfumo.

Ofisi ya TSC Wilayani Kibiti, Mkoani Pwani inahudumia Halmashauri moja ya Kibiti ikiwa na jumla ya shule 101 ambazo kati yake Shule za Msingi ni 77, Sekondari 14, na Shikizi 10 (Usimbe, Nyambele, BETA, Ndungutu, Zimbwini, Nyambangala, Kimbendu, Kibwibwi, Mweyubaruti na Songas), zikihudumiwa na jumla ya Walimu 860 (Wanaume 499 na Wanawake 361) ambao kati yao; Walimu 633 (Wanaume 356 na Wanawake 277) wanafundisha Shule za Msingi huku Walimu 227 (Wanaume 143 na Wanawake 84) wakiwa wanafundisha Shule za Sekondari.

# VIONGOZI TSC WAPATA FURSA KUUFAHAMU UCHUMI WA BULUU ZANZIBAR

**Na Mwandishi Wetu – Zanzibar.**

Viongozi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiongozwa Mwenyekiti na Katibu wa Tume hiyo wamepata fursa ya kuufahamu uchumi wa Buluu wa Zanzibar baada ya kupata wasilisho la mada kuhusu Dhana ya Uchumi wa Buluu Zanzibar iliyowasilishwa na Mhandisi Rashid Mabrouk Ali kutoka Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi Zanzibar.



*Mhandisi Rashid Mabrouk Ali kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar akiwasilisha mada kuhusu dhana ya Uchumi wa Buluu kwenye Mkutano wa Tume uliofanyika hivi karibuni katika ukumbi wa wa jengo la Mamlaka ya Udhibiti Huduma za Maji na Nishati (ZURA) viziwani Zanzibar.*

Mhandisi Rashid aliwasilisha mada hiyo Februari 16, 2022 wakati alipotembelea Mkutano wa Tume uliokuwa unafanyika katika ukumbi wa jengo la Mamlaka ya Udhibiti Huduma za Maji na Nishati (ZURA) kwa lengo la kutoa elimu juu ya uchumi wa bahari unaotambulika kwa jina maarufu la Uchumi wa Buluu.



*Mwenyekiti wa TSC Prof. Willy Komba (katikati), Makamu Mwenyekiti, Bahati Mgongolwa (kushoto) pamoja na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama wakifuatilia mada inayohusu dhana ya Uchumi wa Buluu Zazibar iliyowasilishwa na Mhandisi Rashid Mabrouk Ali kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar. Wasilisho hilo lilifanyika hivi karibuni wakati wa Mkutano wa Tume uliofanyiaka visiwani Zanzibar.*

Mtaalau huyo alianza kwa kueleza kuwa dhana ya Uchumi wa Buluu Zanzibar inajumuisha matumizi endelevu ya bahari na rasilimali zake pamoja na uhifadhi wa mazingira kwa maendelo ya kijamii na kiuchumi.

Alisema kuwa Sekta ya Uchumi wa Buluu Zanzibar inajumuisha sekta za kiuchumi zinazohusiana na maliasili za baharini na ukanda wa pwani ambazo ni pamoja na uvuvi mdogo mdogo wa bahari ya ndani, uvuvi wa bahari kuu, kilimo bahari, ufugaji wa mazao ya baharini, usafiri wa baharini ambao unajumuisha huduma za biashara na usalama katika usafirishaji baharini.

# VIONGOZI TSC WAPATA FURSA KUUFAHAMU UCHUMI WA BULUU ZANZIBAR

Sekta zingine zinazohusika na uchumi huo ni miundombinu ya kimkakati na viwanda katika huduma za bandari, utalii wa baharini na fukwe, nishati mbadala na utafutaji wa madini na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia pamoja na shughuli za michezo ya baharini.

Aliendelea kueleza kuwa katika kuhakikisha malengo ya maendeleo hayo yanafikiwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetayarisha Sera ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2021 ili kusimamia ukuaji wa uchumi wa Zanzibar na matumizi endelevu ya rasilimali za bahari.

Alifafanua kuwa Serikali hiyo imekusudia kupambana na changamoto zinazoweza kuzuia matumizi endelevu ya bahari na rasilimali zake ambazo zinaweza kuwa kikwazo cha kuondoa umaskini kwa wananchi na hivyo kutofikiwa kwa malengo ya uchumi wa buluu.

"Changamoto hizo ni pamoja na uvuvi haramu, mabadiliko ya tabia nchi, usalama wa baharini na uharibifu wa mazingira ya bahari ikiwemo Matumbawe, Mikoko na Nyasi za Bahari," alisema Rashid.

Alihitimisha kwa kueleza kuwa Zanzibar imejipanga vizuri katika kuhakikisha kuwa rasilimali zote zinazopatikana kutokana na bahari zinatumiwa ipasavyo ili kuleta maendeleo kwa wananchi na hivyo Serikali ya Awamu ya Nane chini ya uongozi wa Rais Hussein Mwinyi inawakaribisha wawekezaji wanaoweza kuwekeza katika maeneo mbalimbali visiwani hapo.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba alimshukuru Mhandisi huyo kwa wasilisho lake na kusema kuwa mada hiyo imwewapa picha kubwa ya kuelewa dhana ya uchumi wa buluu ambao ni ubunifu mzuri katika kuimarisha uchumi wa wananchi, serikali na Taifa kwa ujumla.



*Wajumbe na Sekretarieti ya TSC wakifuatilia mada kuhusu Uchumi wa Buluu Zanzibar.*

# TSC MKURANGA YAJIVUNIA KUIMARIKA KWA UTOAJI HUDUMA KWA WALIMU BAADA YA KUPUNGUA KWA MALALAMIKO KATIKA MAENEO MBALIMBALI

**Na. Mwandishi Wetu – Mkuranga**

Imabainika kuwa pamoja na kuwa ndiyo Halmashauri ya Wilaya yenye shule na walimu wengi katika Mkoa wa Pwani, Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga imefanikiwa kuimarisha utoaji huduma kwa walimu na kupunguza kwa kiasi kikubwa malalamiko yao katika maeneo kadhaa ikiwemo madai, kupanda vyeo, uthibitihwaji kazini kwa wakati usiozidi miezi sita kwa waajiriwa wapya kazini na stahiki mbalimbali ziwahusuzo.

Imeelezwa kuwa mafanikio hayo yanatokana na Ofisi ya TSC Wilaya ya Mkuranga kuwa na utaratibu wa kuwatembelea walimu katika vituo vyao vya kazi kwa huduma mbalimbali za kiutumishi ikiwa ni pamoja na kutoa elimu juu ya Sheria, Kanuni, Taratibu, na Miongozo mbalimbali ya utendaji kazi kwa watumishi wa umma kazi iliyofanyika katika shule 13 kati ya 163 zikiwemo shikizi 13 katika kipindi hiki cha nusu mwaka wa fedha 2021/ 22.

Akizungumza na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali Tume Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, hivi karibuni akiwa ziarani katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, na Morogoro, Kaimu Katibu Msaidizi (KKM) wa TSC Mkuranga, Ndg. Mickdad Mickdad alisema; Walimu katika Wilaya ya Mkuranga wamepunguza sana utembeleaji wa Ofisi ya TSC Wilaya kutokana na mahitaji yao mengi na hasa yale ya muda mrefu kutatuliwa na hivyo kutumia muda mwingi katika kutoa huduma vituoni mwao.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mkuranga, Mikidadi Mikidadi akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya TSC ya Wilaya hiyo kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani) wakati mkuu huyo wa kitengo alipotembelea ofisi hiyo hivi karibuni.*

KKM huyo alisema, "Kupungua kwa malalamiko na kuimarika kwa utoaji huduma vituoni kumeimarisha pia hali ya nidhamu hasa kupungua kwa utoro na kushusha kiwango cha mashauri kutoka 19 mwaka 2016/ 17 hadi kufikia 12 mwaka 2020/ 21 na kufikia nusu mwaka wa fedha 2021/ 22 jumla ya mashauri sita tu yamewasilishwa kwetu huku utoro ukiongoza kwa mashauri matano na moja la mwalimu kutotimiza wajibu kama anavyopaswa, ambapo kati ya hayo matano ya utoro; matatu yanasubiri uchunguzi, moja linasubiri kikao, na mawili yameshatolewa uamuzi kwa wahusika kufukuzwa kazi."

KKM Mickdad aliendelea kuwasihi walimu wilayani humo na nchini kwa ujumla kuendelea kufuata miongozo, kutii na kuzizingatia nguzo kuu za kazi ya ualimu sambamba na Sheria, Kanuni, na Taratibu za Tume ya Utumishi wa Walimu kama zilivyoainishwa katika Sheria ya Tume ya Mwaka 2016.

Ofisi ya TSC Wilayani Mkuranga, Mkoani Pwani inahudumia Halmashauri moja ya Wilaya ya Mkuranga ikiwa na jumla ya shule 201 (Serikali 150, Shikizi 13, na Binafsi 38) ambazo kati yake Shule za Msingi ni 143 (Serikali

# TSC MKURANGA YAJIVUNIA KUIMARIKA KWA UTOAJI HUDUMA KWA WALIMU BAADA YA KUPUNGUA KWA MALALAMIKO KATIKA MAENEO MBALIMBALI



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (kushoto) akizungumza na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mkuranga, Mikidadi Mikidadi juu ya maendeleo ya Ofisi hiyo katika kutoa huduma kwa walimu.*



*Baadhi ya Watumishi wa TSC Wilaya ya Mkuranga wakiwa kwenye kikao kilichowakutanisha na Mkuu wa Kitengo cha Mawasilano ya Serikali, Gerard Chami (hayupo pichani). Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC Wilaya ya Mkuranga.*

120 na Binafsi 23), Sekondari 45 (Serikali 30 na Binafsi 15), na Shikizi 13, zikihudumiwa na jumla ya Walimu 1,806 (Wanaume 753 na Wanawake 1,053) ambao kati yao; Walimu 1,236 (Wanaume 452 na Wanawake 784) wanafundisha Shule za Msingi huku Walimu 570 (Wanaume 301 na Wanawake 269) wakiwa wanafundisha Shule za Sekondari.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali na Habari kutoka Ofisi ya Rais – Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami yupo katika mwendelezo wa ziara za Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali na Habari za kila mwezi kutembelea Ofisi za TSC Wilaya zilizopo katika wilaya 139 hapa nchini ili kujionea utendaji kazi na kupata taarifa za utekelezaji wa majukumu ya TSC Wilaya pamoja na kutoa elimu zaidi ya uelewa wa majukumu ya TSC kwa wadau mbalimbali wa Tume.



*Baadhi ya Watumishi wa TSC Wilaya ya Mkuranga wakiwa kwenye kikao kilichowakutanisha na Mkuu wa Kitengo cha Mawasilano ya Serikali, Gerard Chami (hayupo pichani). Kikao hicho kilifanyika hivi karibuni katika ofisi za TSC Wilaya ya Mkuranga.*



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (katikati) akiongea na chombo cha habari cha ZBC juu ya utekelezaji wa majukumu ya TSC. Mahojiano hayo aliyafanya hivi karibuni visiwani Zanziba wakati wa Mkutano wa Tume. Upande wa kulia ni Katibu wa TSC, Paulina Nkwama na upande wa kushoto ni Mwenyekiti Msaidizi wa TSC, Bahati Mgongolwa.*



*Katibu wa TSC, Paulina Nkwama akiwa katika mahojiano na kituo cha runinga cha ZBC wakati wa mkutuano wa Tume uliofanyika hivi karibuni visiwani Zanzibar.*



*Viongozi wa TSC wakiwa katika kipindi cha majadiliano cha runinga kilichohusu utekelezaji wa majukumu ya TSC.*



*Viongozi wa TSC wakiwandaa kipindi cha majadiliano cha runinga kilichohusu utekelezaji wa majukumu ya TSC.*

# MWAMKO DUNI WA WAZAZI NA JAMII WILAYANI LINDI NA MTAMA KATIKA MASUALA YA ELIMU KWARUDISHA NYUMA JITIHADA ZA WALIMU KATIKA UTOAJI HUDUMA

**Na. Mwandishi Wetu – Lindi**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Lindi imelalamikia mwamko hafifu wa wazazi na jamii wilayani humo katika sekta ya elimu hali inayoleta wakati mgumu kwa walimu kutekeleza wajibu wao kwa kiwango kinachotakiwa katika vituo vyao vya kazi.

Akizungumza na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali Tume Makao Makuu, Ndg. Gerard Chami, hivi karibuni akiwa ziarani katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, na Morogoro, Kaimu Katibu Msaidizi (KKM) wa TSC Lindi, Ndg. Azizi Metta, alisema; pamoja na mazingira na tamaduni za mikoa ya pwani kumekua na changamoto kubwa ya mwamko wa duni wa wazazi na jamii katika kujihusisha na kushughulikia masuala mbalimbali ya elimu kwa watoto na ndugu wanaowasomesha jambo linalorudhisha nyuma bidii ya walimu katika usimamizi na utoaji huduma hiyo.

KKM Metta alisema; "Tunajivunia kiutendaji kwa walimu wetu tunaowasimamia ambao ndiyo wanarithisha maarifa kwa wanafunzi wana uwajibikaji uliotukuka mahali pa kazi, ushirikiano mzuri baina yao na wanafunzi, uvumilivu na usikivu katika utumishi wa umma ambao kwasasa unaufanya mkoa



*Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Lindi, Azizi Metta akizunguza na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami katika Ofisi za TSC Lindi hivi karibuni.*



*Baadi ya watumishi wa TSC Wilaya ya Lindi wakiwa katika kikao na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani) wakati wa ziara yake aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.*

wa Lindi kuwa miongoni mwa mikoa inayofanya vema kitaaluma. Tatizo kubwa tunalokabiliana nalo ni mwamko duni wa wazazi na jamii ya wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtama na Manispaa ya Lindi tunaowapa huduma kwa watoto na ndugu zao kuturudisha

# MWAMKO DUNI WA WAZAZI NA JAMII WILAYANI LINDI NA MTAMA KATIKA MASUALA YA ELIMU KWARUDISHA NYUMA JITIHADA ZA WALIMU KATIKA UTOAJI HUDUMA

nyuma kwa kutowajibika kwenye maeneo yao na hivyo kushusha ari ya walimu katika utoaji huduma."

Pamoja na hilo KKM Metta alisema TSC wilaya ya Lindi inayohudumia Halmashauri mbili yaani Mtama na Manispaa ya Lindi inapata ushirikiano mkubwa kutoka kwa halmashauri zote ili kuendelea kupandisha kiwango cha elimu mkoani humo na kuweka mazingira rafiki ya kiutendaji kwa walimu kwani wanashirikishwa katika kuandaa warsha za mafunzo mbalimbali elekezi kwa Maafisa Elimu Kata, Wakuu wa Shule za Sekondari, Walimu Wakuu wa Shule za Msingi, na Walimu wa ajira mpya kila wanapoajiriwa ili kujengeana uwezo na kutekeleza majukumu kwa weledi na ufanisi zaidi.

Akielezea namna ambavyo TSC imekua ikijitangaza kwa walimu na wadau wake wengine ili kukuza uelewa wa majukumu na mipaka ya kiutendaji ya Tume alisema; kwa sehemu kubwa wanatumia vikao vya mabaraza ya madiwani ambao ndiyo wawakilishi wa wananchi katika kata, kufanya ziara zinazoendana na vikao na walimu katika vituo vyao vya kazi, kujiunga na makundi yenye tija kwenye mitandao ya jamii ambako hutoa elimu hususan kwa walimu ambako pia katika kupunguza hoja na malalamiko mambo mbalimbali hujibiwa na kutolewa ufafanuzi kutokana na hoja zinazowasilishwa na maswali yanayoulizwa hasa katika eneo la utumishi.

Vilevile KKM Metta alisema katika mashauri ya nidhamu matatu yaliyopokelewa mpaka sasa kwa halmashauri zote mbili wanazozihudumia kwa mwaka huu wa fedha 2021/ 22; mashauri yote yametoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtama huku ikiwa ni mara ya kwanza kwa halmashauri hiyo kupata na kuwasilisha mashauri tangu kuanza kwake na sehemu kubwa ya mashauri yanayowasilishwa na halmashauri zote yamebainika



*Baadi ya watumishi wa TSC Wilaya ya Lindi wakiwa katika kikao na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (hayupo pichani) wakati wa ziara yake aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.*

# MWAMKO DUNI WA WAZAZI NA JAMII WILAYANI LINDI NA MTAMA KATIKA MASUALA YA ELIMU KWARUDISHA NYUMA JITIHADA ZA WALIMU KATIKA UTOAJI HUDUMA



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasilano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami (wa tatu kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Lindi.*

kusababishwa na walimu kutokua na uelewa wa kutosha juu ya masuala ya wajibu na haki za kiutumishi kwa mtumishi wa umma jambo ambalo limeleta msukumo mkubwa wa uhitaji na mkakati wa kufanya ziara za kuwatembelea vituoni na kutoa elimu katika maeneo hayo yenye upungufu wa weledi ikiwa ni pamoja na kujua Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo ya Utumishi wa Umma, na Nguzo Kuu za Kazi ya Ualimu.

Pamoja na hali hiyo, KKM Metta alisema pamoja na elimu kuendelea kupewa msukumo kwa walimu bado pia Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu hawajatambua vema majukumu na ukomo wa kimaamuzi wa mamlaka zao Kisheria hasa katika mashauri na hivyo kutoa rai kwa Ofisi za TSC nchini kuendelea kwa pamoja kutoa elimu hiyo ya ukomo wa mamlaka zao kisheria kupitia mihadhara mbalimbali, mikutano na vikao vinavyowakutanisha.

Ofisi ya TSC Lindi inahudumia jumla ya Halmashauri mbili; Halmashauri ya Wilaya ya Mtama na Manispaa ya Lindi zikiwa na jumla ya shule 199; Lindi shule 96 ikiwa ni 78 za Msingi na 18 za Sekondari huku Mtama ikiwa na shule 103 ambazo 79 niza Msingi na 24 za Sekondari kwa jumla ya walimu 1,181 (Lindi ikiwa na jumla ya walimu 516; Msingi walimu 280 na Sekondari walimu 236 huku Mtama ikiwa na jumla ya walimu 665; Msingi walimu 495 na Sekondari walimu 170), idadi aliyosema inajumuisha shule tano za binafsi ambapo nne niza msingi na moja ya sekondari (WAMA) ambayo pamoja na walimu wake pia inahudumiwa na walimu wa Umma.

# HAPE, KIRAMA WAAGWA TSC



*Mwenyekiti wa TSC akiwa amebeba zawadi kwa ajili ya kuwakabidhi viongozi wanaoagwa.*

**Na Mwandishi Wetu - Zanzibar**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imewaaga aliyekuwa Kamishna wa Tume hiyo akitokea Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mathew Kirama ambaye aliteuliwa kuwa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma na aliyekuwa Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Christina Hape ambaye mkataba wake wa kufanya kazi TSC umemalizika hivi karibuni.

Hafla ya kuwaaga viongozi hao ambayo ilihudhuriwa na Mwenyekiti, Katibu, Makamishna, Menejimenti na baadhi ya watumishi wa TSC ilifanyika Februari 17, 2022 mjini Zanzibar ambapo ndipo Mkutano wa Tume ulipokuwa unafanyikia.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba alieleza kuwa viongozi hao wamekuwa mfano wa kuigwa kutokana na namna walivyokuwa wakitekeleza majukumu yao kwa bidii, weledi na ubunifu kitu ambacho kimesaidia tume kupiga hatua katika kusimamia Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu.

"Tumefanya kazi vizuri na Kamishna mwenzetu bw. Mathew Kirama na kutokana na uwajibikaji wake, Mhe. Rais aliona kuwa anafaa kumsaidia kazi katika nafasi ya Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma. Tunampongeza sana kwa kuteuliwa kwake kwa sababu tunajua kabisa kwamba Rais alimuona kutokana na utendaji wake wa kazi," alisema Prof. Komba.

Akimzungumzia Bi Christina Hape, Prof. Komba alisema sehemu kubwa ya utumishi wa kiongozi huyo amekuwa katika kufanya kazi za utumishi wa walimu, hivyo uzoefu wake umeisaidia TSC kupiga hatua katika kutoa huduma bora kwa walimu.

"Mkurugenzi Hape naye amekuwa ni nguzo muhimu katika utendaji kazi wa kila siku wa TSC, yeye alikuwepo tangu TSC inaazishwa na hata huko nyuma pia alikuwa akifanya kazi katika vyombo vilivyokuwa vinasimamia utumishi wa walimu. Uzoefu wake umetusaidia hasa sisi Makamishna kuijua tume kwa haraka na kufanya maamuzi yanayohusu maslahi ya walimu kwa ufanisi," alisema Prof. Komba.

Kwa upande wake Katibu wa TSC, Paulina Nkwama alisema viongozi hao walioagwa wamekuwa ni darasa tosha kwa watumishi wengine wa TSC



*Katibu wa TSC akiwa amebeba zawadi kwa ajili ya kuwapatia viongozi waliokuwa wanaagwa.*

# HAPE, KIRAMA WAAGWA TSC



*Viongozi na watumishi mbalimbali wakimzawadia aliyekuwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Christina Hape.*

kutokana na namna walivyokuwa na michango chanya katika kuhakikisha tume inafikikia malengo yake yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria.

"Kwa niaba ya watumishi wenzagu, ninapenda kuwashukuru sana kwa utendaji wenu ambao umeisaidia TSC kuwahudumia walimu kwa namna bora zaidi. Kamishna Kirama ndiye aliyeyekuwa na uzoefu wa muda mrefu zaidi kwenye tume hii kwani hiki kilikuwa kipindi chake cha pili, hivyo uzoefu wake umetusaidia sisi sekretarieti kufanya kazi kwa weledi na ufanisi zaidi," alisema.

Aliongeza kuwa, "Mkurugenzi Hape yeye amekuwa mwalimu kwetu katika msuala ya utumishi wa walimu kwani karibia wajumbe wote wa Menejimenti ya TSC Makao Makuu tumepokelewa naye. Hivyo, kwa kweli tumejifunza mengi kutoka kwakwe na michango yake imeifanya TSC kufika hapa tulipo sasa,".

Kwa upande wake Bw. Mathew Kirama aliwashukuru viongozi na watumishi wote wa TSC kwa ushirikiano waliompatia katika kipindi chote alichokuwa ni mmoja wa makamishna wa tume huku akiahidi kuendeleza ushirikiano kati ya TSC na Tume ya Utumishi wa Umma ambayo anaiongoza kwa sasa.

"Ninawashukuru sana ndugu zangu kwa heshima hii mliyotupa, hii inadhihirisha kuwa tulifanya kazi vizuri na kwa umoja. Binafsi, nimejifunza mengi kutoka TSC ambayo yatanisaidia kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi zaidi. Lakini napenda niahidi kuwa ushirikiano huu uliokuwepo kati yangu na ninyi nitaendelea kuudumisha ili tuwe tunashirikiana na kubadilishana uzoefu mara kwa mara kwa ustawi wa taasisi zetu na wale tunaowahudumia", alisema Kirama.

Naye Bi Christina Hape alisema kuwa katika kipindi chote alichokaa katika tume hiyo aliona kuwa siri kubwa ya mafanikio yaliyopatikana ni upendo miongoni mwa watumishi na viongozi kitu ambacho kimefanya kazi zifanyike kwa ubora bila kuwa na mivutano isiyokuwa na tija.

Kiongozi huyo aliwasihi watumishi wote waendeleze utamaduni huo wa kufanya kazi kwa kushirikiano na upendo ili TSC iweze kuongeza kasi zaidi katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili walimu na kuwafanya walimu waendelee kuwahudumia wanafunzi kwa ukamilifu.



*Aliyekuwa Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Christina Hape (aliyeshika fedha) akitokwa na machozi ya furaha baada ya kupokea zawadi kutoka kwa viongozi na watumishi wa TSC huku watumishi na viongozi hao wakiendelea kuserebuka.*

# HAPE, KIRAMA WAAGWA TSC







*Viongozi mbalimbali wakiserebuka wakati wa hafla ya kuwaaga Bw. Mathew Kirama na Bi Christina Hape.*

# TSC MOROGORO: TUNAHITAJI USHIRIKIANO ZAIDI KUTOKA KWA WAAJIRI

**Na Mwandishi Wetu - Morogoro**

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Morogoro, Lusubilo Mwaisunga amehimiza kuongezeka kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya TSC wilayani hapo na Ofisi za Waajiri wa Walimu katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ili kuendelea kutatua changamoto za walimu kwa wakati.



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Morogoro, Lusubilo Mwaisunga (kulia) akiongea na Mkuu wa Kitengo cha Mwasiliano ya Serikali kutoka TSC Makao Makuu, Gerard Chami kuhusiana na utekelezaji wa Majukumu ya TSC katika Wilaya ya Morogoro.*

Mwaisunga ametoa kauli hiyo hivi karibuni akiwa ofisini kwake wakati wa mazungumzo yake na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Gerard Chami yaliyolenga kufahamu maendeleo yaliyofikiwa na ofisi hiyo katika kutoa huduma kwa walimu.

"TSC hapa Wilaya ya Morogoro tunahudumia Halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Manispaa na Halmashauri ya Wilaya. Manispaa ya Morogoro ina jumla ya Shule za Msingi 72 na Shule za Sekondari 27. Halmashauri ya Wilaya nayo ina shule 158 za msingi na 29 za Sekondari zinazoshughulikiwa na TSC kwa mujibu wa sheria," alisema.



*Mkuu wa Kitengo cha Mwasiliano ya Serikali, Gerard Chami akielezea jambo kwa Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Morogoro, Lusubilo Mwaisunga hivi karibuni katika ofisi za TSC Wilaya ya Morogoro.*

Aliongeza kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro ina jumla ya walimu 1831 ambapo katika idadi hiyo walimu 1256 ni wa shule za msingi na 575 wakiwa ni wa shule za sekondari huku Manispaa ya Morogoro ikiwa na jumla ya walimu 3368 ambapo katika idadi hiyo walimu 2154 ni wa shule za sekondari na 1214 ni wa shule za msingi.

Alifafanua kuwa walimu hao ambao wanachukua idadi kubwa ya watumishi wa umma katika wilaya hiyo ili waweze kuhudumiwa vizuri na kwa wakati ni lazima kuwe na ushirikiano wa

# TSC MOROGORO: TUNAHITAJI USHIRIKIANO ZAIDI KUTOKA KWA WAAJIRI



*Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Morogoro, Lusubilo Mwaisunga akimwonesha Mkuu wa Kitengo cha Mwasiliano ya Serikali, Gerard Chami hali ya ofisi za TSC Wilaya ya Morogoro ambapo ameomba kupatiwa makabati ya kuhifadhia nyaraka. Wengine ni Watumishi wa TSC Wilaya ya Morogoro.*

karibu kati ya ofisi ya TSC na ofisi za waajiri kwa kuwa ndio wenye jukumu kubwa la usimamizi wa masuala ya walimu.

"Pamoja na kwamba tunashirikiana na ofisi za waajiri katika masuala mbalimbali ya utumishi wa walimu, bado tunahitajika kuongeza juhudi zaidi ili tuongeze ushirikiano na mawasilino kwa kuwa changamoto za walimu bado zipo na zinahitaji utatuzi wa haraka," alisema kiongozi huyo.

Ameendelea kusema kuwa, "haipendezi ukiomba taarifa za walimu huzipati kwa wakati, au mwalimu ahamishwe kituo cha kazi bila TSC kupewa taarifa, au maandalizi ya bajeti ya walimu yanafanyika lakini TSC hajui kinachoendelea. Tusiposhirikiana tunaweza kujikuta tunakuwa kero kwa walimu badala ya kuwa



*Mtumishi wa TSC Wilaya ya Morogoro Majubu Mkama.*

suluhu ya matatizo yao."

Lusubilo alisema kwamba kuna haja kwa viongozi wanaoshughulikia masuala ya elimu na utumishi katika wilaya hiyo kupata fursa ya kuijua kwa undani sheria ya TSC na kanuni zake ili kuepusha mwingiliano wa majukumu katika utendaji wa kazi.

Alisema kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448, TSC ndiyo mamlaka ya ajira na nidhamu kwa walimu, hivyo inapokuja suala la kumchukulia mwalimu hatua za nidhamu, Mkuu wa Shule au TSC ngazi ya Wilaya ndio wenye jukumu kuchukua hatua hizo kulingana na aina ya kosa kama ilivyoelekezwa na sheria.

"Tumekuwa tukielimishana na wenzetu juu ya mipaka ya majukumu na mamlaka ya TSC kwa mujibu wa sheria. Kule Halmashauri ya Wilaya kuna waalimu waliazimiwa kusimamishwa kazi na baraza la madiwani na wakasimamishwa kazi kitu ambacho ni kinyume na sheria. Tumeendela kukaa na wenzetu kupeana elimu na sasa kwa kweli tunasogea tofauti na siku za nyuma," alisema Lusubilo.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo alihitimisha kwa kusema kuwa walimu wengi wana hamu ya kupata elimu ya masuala mbalimbali ya utumishi wao kwa kuwa wengi wao bado hawazifahamu sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma, hivyo ofisi ya TSC inaendelea kuwafikia walimu hao kwa namna mbalimbali ili kuwapatia elimu.



*Makamishna na Sekretarieti ya TSC wakifurahia elimu juu ya zao Kungumanga wakati walipotembelea moja ya mashamba ya mimea mbalimbali visiwani Zanzibar.*



*Makamishna na Sekretarieti ya TSC wakipata elimu juu ya zao la Vanila wakati walipotembelea moja ya mashamba ya mimea mbalimbali visiwani Zanzibar.*



*Makamishna na Sekretarieti ya TSC wakipata elimu juu ya zao la Kokoa wakati walipotembelea moja ya mashamba ya mimea mbalimbali visiwani Zanzibar.*




**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz* **Tovuti:** *www.tsc.go.tz*

***Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania*** ***tumeyautumishiwawalimutanzania***